

CHUO KIKUU CHA MTAKATIFU AGUSTINO

Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma
S.L.P. 307 MWANZA, TANZANIA



MAHAFALI YA KUMI NA NANE (18)

Mkuu wa Chuo cha Mtakatifu Augustino Tanzania (SAUT) Mhashamu Baba Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa wa jimbo Katoliki la Iringa, anayofuraha kuwatangazia wanafunzi wote wanaohitimu masomo yao chuoni kwa mwaka wa masomo 2015/2016 kwamba, mahafali ya kumi na nane (18) yatafanyika katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino kwenye viwanja vya Raila Odinga kuanzia saa 3:00 asubuhi.

Tarehe za Mahafali ya kumi na nane (18):

1. Ijumaa: Tarehe 16/12/2016.
Wahusika: Kitivo cha Elimu na Kitivo cha Sayansi ya jamii na Mawasiliano.
2. Jumamosi: Tarehe 17/12/2016.
Wahusika: Kitivo cha Sheria, Kitivo cha Biashara na Utawala, Kitivo cha Uhandisi na Postgraduate Programmes.

Wahitimu wote wanatakiwa kufanya yafuatayo:

1. Wahitimu wote wanatakiwa kulipa Tshs. 52,000/= (elfu hamsini na mbili tu) kupitia akaunti ya chuo namba 015101001461 NBC. Wahitimu wanatakiwa kuchukuwa majoho kuanzia siku ya Jumatatu tarehe 12/12/2016 - 15/12/2016 saa 3:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.
2. Majoho lazima yarudishwe ndani ya siku mbili (2) baada ya mahafali, vinginevyo kutakuwa na faini ya shilingi 10,000/= kwa kila siku itakayozidi.
3. Wahitimu wanatakiwa kufika chuoni tarehe 15/12/2016 saa 9:00 alasiri kwa ajili ya taratibu zinazotakiwa ikiwa ni pamoja na kufanya mazoezi kwa ajili ya mahafali.
4. Wahitimu wote wanatakiwa kufanya maandalizi yote ya usafiri na malazi wenyewe kwa kipindi chote cha shughuli za mahafali.

WOTE MNAKARIBISHWA


Dr. Negussie Andre D.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma

Tel: +255 736 200943, Fax: +255 28 2550167, Email: dvcaa@saat.ac.tz

